# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS-TAMISEMI

# HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

# NYERERE HIGH SCHOOL - MIGOLI

**S.L.P. 240,**

**IRINGA.**

**Namba za simu**

Mkuu wa shule **0768 711 145**

Makamu mkuu wa shule **0752 160 384**

Taaluma **0769 065 982**

Malezi **0769 528 876**

Mhasibu **0755 834 274**

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi ___________________________________

S.L.P _______________

___________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI** NYERERE HIGH SCHOOL-MIGOLI **HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA, MKOA WA IRINGA KWA MWAKA 2021/2022.**

## 1.0 UTANGULIZI

Kwa niaba ya Jumuiya ya **Nyerere High School-migoli**, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na shule yetu. Kuchaguliwa kwako kumezingatia mafanikio uliyoyapata katika kumaliza elimu ya kidato cha Nne na matokeo yako mazuri katika mtihani wa Taifa. Shule hii inapokea wanafunzi mchanganyiko wa kutwa kwa kidato cha I hadi IV na bweni kwa kidato cha V na VI ambao ni wavulana tu. Hata hivyo zipo nafasi chache za hostel kwa kidato cha I- IV. Nafasi hizo hutolewa kwa wale tu wenye shida ya mahali pa kuishi hapa Migoli. Michepuo inayofundishwa katika shule hii kwa kidato cha tano ni, **HGL, HGK, HKL, EGM** na **HGE**.

Shule yetu itafunguliwa tarehe **05.07.2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **12.07.2021** Siku ya kuripoti utatakiwa kufika shuleni na kusajiliwa tayari kwa masomo. Wakati wa kusajiliwa utatakiwa kulipa ada ya shule na kuthibitisha kuwa umetimiza masharti mengine yote kama inavyoonesha katika barua hii.

Jaza fomu zote zilizoambatanishwa na uje nazo na kukabidhi wakati wa kusajiliwa. Michepuo inayofundishwa katika shule hii kwa kidato cha tano na cha sita ni, **HGL, HGK, HKL, EGM** na **HGE**.

## 1. 1 MAHALI SHULE ILIPO

**Nyerere High School-Migoli** ipo kijiji cha **Migoli** Halmashauri ya **Wilaya ya Iringa.**

Kwa kutokea **Iringa mjini**, shule ipo umbali wa **km 92** barabara ya **Iringa-Dodoma** katika kijiji cha **Migoli.** Vilevile kwa upande wa kutokea **Dodoma jiji**, shule ipo umbali wa **km 162** barabaraya **Dodoma - Iringa** katika kijiji cha **Migoli.**

### 1.2 Usafiri

Usafiri wa basi kutoka **Iringa** unapatikana stendi kuu ya zamani ya mabasi **Iringa-Mjini** na stendi kuu mpya ya mabasi ya **Mkoa wa Iringa** iliyopo **Igumbilo**. Nauli yake ni Tsh **5,000/-**

Usafiri wa basi kutoka **Dodoma** unapatikana stendi ya mabasi ya **Mkoa wa Dodoma** iliyopo **Nane nane**. Nauli yake ni Tsh **10,000/-** Kituo cha kushukia ni **Migoli**

**Karibu sana Nyerere High School-Migoli, nakutakia safari njema ya kuja hapa**.

## 2. 0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE.

a) Suruali mbili za kaki zenye linda(kitambaa kaki namba moja)
*b)* Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
c) Sare za michezo kwa shule hii ni jezi rangi nyekundu(Full) moja na viatu vya michezo.
d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
e) Soksi jozi mbili nyeupe.
f) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
g) Sweta yenye shingo V rangi ya bluu.
h) Track suti rangi ya kijani yenye ufito mweupe.
i) Nguo za kushindia (shamba dress) T-shirt rangi ya **njano(zito isiyo na maandishi wala michoro)** na suruari **dark blue** kitambaa kizito.
j) T-shirt **nyeupe** yenye nembo ya shule inapatikana shule kwa sh. 10,000/=

### 2.2 ADA NA MICHANGO YA SHULE

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI (Tsh) |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya shule | 70,000/- (Kwa muhula 35,000/-) |
| 2 | Ukarabati wa samani | 15,000/- |
| 3 | Kitambulisho | 6,000/- |
| 4 | Taaluma | 30,000/- |
| 5 | Kuwalipa wapishi na walinzi | 30,000/- |
| 6 | Matibabu | 10,000/- |
| 7 | Mtihani ya pamoja(Joint Exams) | 20,000/- |
| 8 | Tahadhari (Hairudishwi) | 7,000/- |
| | **Jumla ya michango** | **188,000/-** (Kwa muhula wa I **153,000/-)** |

**TANBIHI:** Michango yote ilipwe katika akaunti ya shule yenye nambari **60501100060** benki ya **NMB** kwa jina la akaunti: **NYERERE HIGH SCHOOL-MIGOLI.** (**Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip**).

**2.3 MAHITAJI MENGINE MUHIMU :**

i. Rimu za karatasi bunda 2 (kwa mwaka)
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika vimeambatanishwa.
iii. Scientific calculator kwa wanafunzi wenye tahasusi za EGM na HGE
iv. Godoro la sponji la DODOMA (2 ½ x 6) lenye ujazo wa nchi 3 ½
v. Mashuka pair 2 rangi ya pink na chandarua 1.
vi. Vyombo vya chakula (sahani,bakuli, kijiko na kikombe)
vii. Ndoo moja ya lita 20 na moja ya lita 10 zenye mifuniko.
viii. Tochi moja(ya kuchajiwa kwa jua) endapo kukiwa na tatizo la umeme.
ix. Vifaa mahususi kwa kila Tahasusi

| S/N | TAHASUSI | VIFAA |
|---|---|---|
| 1 | EGM | Sululu 1 yenye mpini |
| 2 | HGE | Mapanga 2 na Mpini 1 wa Jembe |
| 3 | HGK | Shoka 1 lenye mpini |
| 4 | HGL | Brashi ngumu ya chooni 1, soft bloom 1 na water squeezer 1 |
| 5 | HKL | Brashi ngumu ya chooni 1, soft bloom 1 na water squeezer 1 |

**3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Kufuga ndevu
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji sigara.
ix. Uasherati, ushoga, kuoa au kuolewa.
x. Kushiriki kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au vifaa vinavyohusiana na simu ya mkononi kama laini chaja n.k katika mazingira ya shule(***kabla ya kufukuzwa shule mwanafunzi,mzazi/mlezi atatakiwa kulipa gharama za uharibifu wa miundombinu ya shule***)
xv. Kudharau bendera ya taifa na alama zingine za taifa
xvi. Kufanya jaribio la kujiua au kutishia kuua
xvii. Uharibifu wa mali za umma kwa makusudi

**TANBIHI ***

- Nguo za michezo zitatumika uwanjani tu na sio mazingira mengine ya shule.
- Nywele ni sehemu ya sare ya shule, zinatakiwa ziwe fupi za kuchana, aidha kucha ziwe fupi na safi wakati wote.
- Hairuhusiwi kuvaa bangili (kacha), au mapambo ya aina yoyote ile shuleni

**Mavazi ya aina nyingine nje ya haya yaliyotajwa hapo juu hayaruhusiwi kabisa shuleni, mwanafunzi atakaye pokelewa ni yule atakaye kuwa amevaa sare za shule zilizo ainishwa hapo juu.**

**MWISHO**

Maagizo yote yatakaguliwa siku ya kuripoti shuleni. Mwanafunzi hatapokelewa endapo hatakuwa amekamilisha maagizo yaliyomo ndani ya fomu hii. Ukifika shuleni utasomewa tena sheria, kanuni na taratibu za shule hii. Ni wajibu wako kutii na kuzifuata kikamilifu. Ukikosa utaonywa kwa maandishi/mdomo au utaonywa kwa kupewa adhabu na ikilazimu utasimamishwa masomo kwa muda (suspension) au kufukuzwa shule kabisa ikibidi kwa mujibu wa sheria.

Mwisho kabisa nachukua nafasi hii tena kukukaribisha sana hapa **Nyerere High School- Migoli** na ni matarajio yangu kuwa ufikapo hapa utaitumia vema fursa hii muhimu uliyotunukiwa na Taifa lako kwani wengi wameikosa.

***Tafadhali mwanafunzi aje na mzazi/mlezi siku ya kusajiliwa hapa shuleni na kuhakikisha fomu zilizoambatanishwa na fomu hii zinajazwa kwa usahihi.***

**MANGA, L**
**MKUU WA SHULE**

**ORODHA YA VITABU AMBAVYO MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJANAVYO KULINGANA NA TAHASUSI YAKE**

**VITABU VYA HISTORY:**

1. How Europe underdeveloped Africa by Walter Rodney.
2. Africa since 1800, 4th edition by Roland Olive and Atmore.
3. The political economy, imperialism by Nabudere.
4. Mastering Advanced level History book II by Kato.
5. World History Advanced Level by Samweli Mhajida.
6. Focus on modern world History History Advanced Level by Chakupewa.J etal (2012) paper I na Paper II.
7. Contemporary history events volume one first edition by Shibitali C.K
8. Major Events in the World History paper 2 Advanced Level Gervas.M Zombwe.

**VITABU VYA UCHUMI:**

1. Economic simplified East Africa Edition by N.A Saleem.
2. Ambilikile Advanced economic paper I.

**VITABU VYA GEOGRAPHY;**

1. Bunnett (2006) physical geography in diagram for Africa Longman Limited china.
2. Economic geography by Mogarn.
3. Human and economic geography by D.T Msabila.
4. The essential of practical geography Advanced level by Joseph William Njiku (2005).
5. Certificate of Human and economic Geography. By Morgan and Leong Chang.

**VITABU VYA KISWAHILI**

**A. USHAIRI:**

1. Kimbunga - G.Gora (Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili) 1999.
2. chungu Tamu-T.A Mvungu (Tanzania published house) 1985.
3. Mapenzi bora-S.Robert (Mkuki na Nyota) 2003.
4. Fungate ya Uhuru M.S Khatibu.

**B. RIWAYA;**

1. Vuta n’ Kuvute- A.Shafi (Mkuki na Nyota)-1999.
2. Kufikilika S.Robert-2003
3. Mfadhili Hussein Tuwa.
4. Usiku utakapokwisha-Mbunda Msokile-2007

**C. TAMTHILIA;**

1. Moran -E.Mbogo
2. Kivuli Kinaishi Said Mohamed-2007.
3. Kwenye Ukingo wa Thim-E.Ussein
4. Nguzo Mama-1982.

**ENLISH LANGUAGE**

1. New advanced level English by Charles. E
2. Advanced level English, A practical approach by Nicholous Asheli.
3. Advanced level literature by Nyambari Nyangwine.
4. Advanced level Learners Dictionary.
5. Teaching English as a foreign language by G.Broughton.
6. English form V and VII by M. Kadege.
7. Contemporary English for advanced level by Francis Mnyawe.
8. Complete course by M.Kadege.

**B-NOVEL:**

1. The beautiful ones are not yet born by A.K Amah.
2. A man of the people by C.Achebe.
3. Divine providence – Mkuki na Nyota.
4. Encounters from Africa – Macmillan.
5. The rape of the peal-Macmillan.

C-**PLAYS/DRAMA;**

1. An Enemy of the people – H.Ibsen.
2. I Will Marry When I want-EAEP
3. Rwanda Magere by Okoti Omtatah-1991
4. The Pride – EAEP
5. Black Mamba-EAEP.

C-**POETRY;**

1. Selected poem from institute of education.
2. The wonderful Surgeon and other poem-Mkuki na Nyota.

**PURE MATHEMATICS;**

1. Pure mathematics I and II by J, K Backhouse.
2. Advanced level pure mathematics by Kinunda.
3. Advanced level pure mathematics by C.J Tranter- 2006
4. S.Chand mathematics for class XI, volume I and II by H.K DASS R.VERMA 2013
5. Calculator Casio.

**BASIC APPLIED MATHEMATICS (BAM):**

1. Basic applied mathematics for Advanced school form V and VI by Septine

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**NYERERE HIGH SCHOOL- MIGOLI**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA TANO**

(sehemu ya kwanza ya fomu hii ijazwe na mwanafunzi na sehemu ya pili ijazwe na mzazi ua mlezi)

| |
|---|
| **Picha** |

## SEHEMU YA KWANZA

(sehemu hii ijazwe na nwanafunzi mwenyewe)

Mimi____________________(mwanafunzi) kwa hiari yangu nakubali nafasi naahidi kutoshiriki/kuanzisha migomo, fujo na makosa ya jinai na nitafuata sheria zote za shule.

Jina la mwanafunzi_______________________________________

Sahihi ya mwanafunzi_________________

Tareh_____/_____/201___

## SEHEMU YA PILI

(Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi)

Mimi______________________________mzazi/mlezi* wa ________________________________

Nakubali/ sikubali* nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda wote awapo shuleni atalazimika kuwa mtii kwa walimu, wazazi, viongozi na jamii kwa ujumla. Atalazimika kufuata sheria zote za shule. Naahidi kuwa mwanangu atazifuata taratibu zote za shule hadi atakapo maliza shule.

Jina la mzazi/mlezi*________________________________________

Sahihi __________________

Tarehe____/____/20_____

***Futa isiyohusika**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**NYERERE HIGH SCHOOL- MIGOLI**
**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI**
(Fomu hii ijazwe na Mzazi/mlezi)

1. Jina kamili la Baba/ Mama/Mlezi*_____________________________________________
2. Namba ya kitambulisho cha NIDA________________________________
3. Elimu yake _________________________________________________
4. Kazi yake ___________________________________________________
5. Namba ya simu _______________________________________________
6. Anuani ______________________________________________________
7. Barua pepe ___________________________________________________
8. Mahali anapoishi Mtaa/Kijiji _____________________________________
9. Wazazi wanaishi pamoja? NDIYO ☐ HAPANA ☐
10. Mtoto anaishi na BABA ☐ MAMA ☐ MLEZI ☐
11. Wazazi wote ni wazima? NDIYO ☐ HAPANA ☐ Kama Hapana, mzazi yupi amefariki?_______________________________________________________
12. Tarehe ya kuzaliwa ya mwanafunzi _____________________________________
13. Namba ya cheti cha kuzaliwa __________________________________________
14. Dini ya mzazi/mlezi*_________________________________________________
15. Dhehebu _________________________________________________________
16. Anuani kamili ya sehemu ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo kama ni nje ya eneo ambalo mzazi/mlezi anakaa ______________________________________________
17. Mimi____________________________________________________mzazi/mlezi* wa __________________________________nakiri kuwa taarifa nilizozitoa hapo juu ni sahihi. Naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi, na mwenye bidii.

**NB:** ***Hakikisha unaambatanisha nakala ya kitambulisho cha*** **NIDA kama kipo**

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**NYERERE HIGH SCHOOL –MIGOLI**
MEDICAL EXAMINATION FORM
**(To be completed by medical officer in respect with a new student)**

Full name_______________________________________

Age ___________________________________________

1. Blood count (red and white)_____________________________________________________
2. Urine examination _______________________________________________________
3. Stool examination _______________________________________________________
4. Syphilis _______________________________________________________________
5. T. B Test ______________________________________________________________
6. Ear Test_______________________________________________________________
7. Eye Test_______________________________________________________________
8. Spleen ________________________________________________________________
9. Abdomen ______________________________________________________________
10. Additional information or any other physical, mental, hereditary of infectious diseases

_________________________________________________________________________________

Treatment after examination

_________________________________________________________________________________

**MEDICAL CERTIFICATE**

I certify that the above concerned has been examined and found **fit/not fit*** to pursue for further education.

Signature_________________

Designation_________________________________________________

Station ____________________________________________________

(Official stamp)

Date_____/____/20___

**NB**. Fomu hii ijazwe na mganga katika hospitali inayotambulika na serikali **(sio zahanati)**

*Erase unwanted information